KAULI YA YOUTH ACTION VOLUNTEERS (04/06/2008) JUU YA

KIFO CHA MAMA MJAMZITO MWANANYAMALA HOSPITALI

Tumepokea na kufuatilia habari za kifo cha mama mjamzito (Teddy Kimoso) na kichanga wake wakati wa kujifungua kwa masikitiko makubwa sana. Imeelezwa kifo hiki kilitokea hospitali ya Mwananyamala hivi karibuni kwa sababu zilizoelezwa na Utawala wa Hospitali hiyo kuwa ni ukosefu wa aina fulani ya dawa. Usiku wa tarehe 3/06/2008 televisheni moja ilirusha taarifa za baadhi ya ndugu wa marehemu wakidai kuwa hawakumtuma mwandishi Jackson Odoyo wa gazeti la Mwananchi kuandika taarifa hizo na kwamba hawana malalamiko yoyote kuhusu kifo cha ndugu yao. Taarifa nyingine zinaendelea kudai kuwa hospitali ya Mwananyamala walitoa sharti la kutokutoa mwili wa marehemu kwa wanandugu mpaka wakanushe kuwa kifo kilitokana na uzembe.

Bila kujali malumbano na siasa zinazoendelea kuhusu kifo hiki, tunawajibika kujadili usahihi wa kilichotokea na mazingira yake.

Tunaelewa kwamba;

- Kwa mujibu wa taarifa kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Hospitali ya Mwananyamala imepangiwa pesa za dawa peke yake shilingi 174,502,463 katika mwaka wa fedha 2007/08
- Kwa mujibu wa Mwongozo wa Utekelezaji wa Sera ya Wananchi Kuchangia Gharama za Huduma za Afya katika Hospitali ya mwaka 1994, Hospitali ya Mwananyamala inakusanya pesa kutoka kwa wananchi kwa utaratibu wa Uchangiaji gharama
- Kwa mujibu wa Mwongozo wa Utekelezaji wa Sera ya Wananchi Kuchangia Gharama za Huduma za Afya katika Hospitali ya mwaka 1994 na Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007, Huduma za mama wajamzito na watoto chini ya miaka 5 ni bure katika nchi yetu ya Tanzania
- Kwa mujibu wa kifungu namba 14 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, kila mtu anayo Haki ya Kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake
- Kwa mujibu wa Mpango wa Utoaji huduma za Afya (CCHP) wa Manispaa ya Kinondoni mwaka wa fedha 2007/08, Hospitali ya Mwananyamala ilipanga kutumia shilingi 22,000,000 kugharamia dawa na vifaa vingine kwa kitengo cha Uzazi hospitalini hapo ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka asilimia 15 hadi 10. Pia ilipanga kutumia shilingi 210,000,000 kujenga jengo la ghorofa moja kwa ajili hiyo.
- Mwaka 2007 magazeti yaliandika mara nyingi juu ya huduma duni katika Hospitali ya Mwananyamala, lugha chafu, malalamiko ya mama wajawazito, mama wajawazito kuchelewa kuhudumiwa wakati wanapokwenda kujifungua, msongamano wa wagonjwa, ukosefu wa dawa na vifaa.

Tunasikitika kwamba;

- Teddy Kimoso alifariki kutokana na ukosefu wa dawa jambo ambalo liko ndani ya uwezo wa hospitali ya Mwananyamala na Manispaa ya Kinondoni

- Manispaa ya Kinondoni inaona ni jambo la kawaida kuelezea umma kwamba ilikuwa halali Teddy Kimoso kufariki kutokana na ukosefu wa dawa ambazo hospitali ina uwezo wa kuzinunua kutoka kwenye fungu la bajeti ya dawa au kutokana na mapato ya uchangiaji wa gharama za matibabu hospitalini Mwananyamala.
- Manispaa ya Kinondoni na Hospitali ya Mwananyamala wanashughulikia tatizo hili kisiasa kwa kuhamasisha propaganda kwamba marehemu hakufa kwa uzembe.

Tunahitaji kuona kwamba;

- Inaundwa tume huru kuchunguza matatizo na vifo vya mama wajawazito na watoto chini ya miaka 5 katika Jiji la Dar es Salaam. Mama wote waliojifungua tangu January 2007 (au ndugu wa marehemu) ni vizuri wakahusika kuhojiwa.
- Manispaa ya Kinondoni inaomba radhi kwa wananchi wa Manispaa hiyo kwa uzembe huo ambao sisi tunafikiri umesababishwa na utawala usio makini katika kulinda maisha ya wananchi
- Manispaa ya Kinondoni iweke wazi ni dawa zipi zilikosekana na kwa sababu gani
- Manispaa ya Kinondoni inawajibisha wote waliohusika
- Manispaa ya Kinondoni itangazia wananchi wake hatua zinazochukua kuhakikisha kwamba vifo havitokei katika sehemu za kutoa huduma za afya kwa sababu zinazozuilika
- Manispaa ya Kinondoni itangazie wananchi jinsi pesa za dawa za mwaka wa fedha 2007/08 zilivyotumika
- Manispaa ya Kinondoni itangazie wananchi kwa lugha rahisi kuhusu makusanyo na matumizi ya pesa za uchangiaji gharama za huduma za afya katika Hospitali ya Mwananyamala
- Baadhi ya wanafamilia wa marehemu Teddy Kimoso waelewe kwamba marehemu alikuwa ndugu yao lakini uhai wa kila raia wa nchi hii ni jukumu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia waelewe kwamba marehemu ndugu yao alistahili kupata huduma bora ikiwa ni pamoja na dawa bure kwa mujibu wa sera tulizoainisha hapo juu.
- Waandishi wa habari wanalindwa katika kuibua ukiukaji wa haki za binadamu unaopelekea vifo kama huu wa vifo vya akina mama.
- Manispaa ya Kinondoni haitumii vitisho na propaganda kutisha wananchi wanaojaribu kutetea haki na uhai wa wananchi
- Manispaa inatoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya haki zao za huduma ya afya zinazotambulika kisera, kisheria na kikatiba
- Nakala za mpango na bajeti ya utoaji huduma kwa kila Hospitali, Kituo cha Afya, na Zahanati zibandikwe sehemu ya wazi wananchi na wahudumu wa afya wafuatilie.

Imetolewa na Youth Action Volunteers (YAV) na Kusainiwa na

Irenei Kiria

Mr. Irenei Kiria
Mkurugenzi Mtendaji
2666355/57

YAV